**HALMASHAURI YA WILAYA USHETU**
**KATA YA UYOGO**
**SHULE YA MSINGI NSUNGA**
**MTIHANI WA MUHULA WA PILI - NOVEMBA, 2025**
**SOMO: SAYANSI NA TEKNOLOJIA DARASA LA TATU**

**JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………………………….**

**SEHEMU. A.**

**1.chagua herufi ya jibu sahihi na uandike katika nafasi uliyopewa**

(i) Ogani inayotumika kuhisi vitu ni ..........(A)ulimi (B)pua (C)ngozi (D)sikio ( )
(ii) Tawi la sayansi linalohusu viumbe hai ni ........(A)fizikia (B)Biolojia (C) kemia (D)mwanasayansi ( )
(iii) Maarifa yanayopatikana kwa njia ya kufanya uchunguzi na majaribio hujulikana kama ......(A)hisabati (B)Lugha (C)udaktari (D)sayansi (
(iv) Mfano wa wanyama ambao ni amfibia ni _________(A)chura (B) mamba (c) kenge (D)Kobe ( )
(v) Sehemu ya mmea ambayo kazi yake ni kufyonza maji na virutubisho kutoka kwenye udongo ni....(A)shina (B)mizizi (C)jani (D)ua ( )

**2.Oanisha fungu A na B ili kupata jibu sahihi kwa kuandika herufi ya jibu sahihi.**

| No | **FUNGU A** | **MAJIBU** | **FUNGU B** |
|---|---|---|---|
| I | Sepali,petali,kikonyo | | (A) Milango ya fahamu |
| Ii | Mvinje na mfeni | | (B)Ogani inayotumika kupata ladha ya chakula. |
| Iii | Mizizi,shina,jani | | (C)Sehemu za ua. |
| Iv | Pua ,ngozi na sikio | | (D)Sehemu za mimea . |
| V | Ulimi | | (E)Mfano wa mimea isiyotoa maua. |
| | | | (F) uchunguzi wa kisayansi |

**3.Chagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku na kujaza kwenye nafasi zilizo wazi** .

| |
|---|
| **,Fizikia , vifaa vya tehama, maabara ,hatua za uchunguzi wa kisayansi , Taaluma za kisayansi** |

(i) Tawi la sayansi linalohusu uhusiano wa maada na nishati_________________________
(ii) Redio ,televisheni,na simu _____________
(iii)Chumba au jengo maalumu linalotumika kufanya majaribio ya kisayansi __________________
(iv)Udaktari , ualimu ,na uhandisi_______________________________
(v) Kubaini tatizo,kubuni dhanio,kuandaa mahitaji ya jaribio ____________________________

**SEHEMU B**

4. **Soma kifungu cha habali kifuatacho na kisha jibu maswali**

Jicho la binadamu limeundwa na sehemu kuu mbili amabazo ni sehemu ya ndani na nje.sehemu ya nje imeundwa na nyusi ,vifuniko vya jicho ,na kope.Sehemu ya ndani imeundwa na mboni au Irisi ,pupili,lenzi ,na Retina .pupili huruhusu mwanga kuingia ndani ya jicho ,mboni hurekebisha kiwango cha mwanga kinachoingia kwenye jicho kwa kutanuka na kusinyaaa ,Retina hupokea mwanga

**Maswali**

(i) Taja sehemu kuu mbili za jicho________________________na ____________________


(ii) Ni sehemu gani huruhusu mwanga kupita kuingia ndani ya jicho________________________

(iii)_________________________hurekebisha kiwango cha mwanga kinachoingia kwenye jicho

(iv) Sehemu za ndani ya jicho ziko ngapi__________________________

(v) Katika habali uliyosoma ni mlango upi wa fahamu unaozungumziwa ____________________

**5. CHUNGUZA MCHORO UFUATAO KISHA JIBU MASWALI YAFUATAYO**




(i) Herufi A inawakilisha __________________________

(ii) Sehemu ambayo kazi yake ni kushikilia majani maua na matunda imeonyeshwa kwa herufi gani ?______________________

(iii) Sehemu ambayo kazi yake ni kutengeneza chakula cha mimea imeonyeshwa kwa herufi gani?____________________________

(iv) Kazi ya sehemu iliyoonyeshwa kwa herufi D ni ___________________

(v) Taja sehemu zilizo onyeshwa kwa harudi (A),______________ (C)_______________ (D)____________